

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA PILI

01 APRILI, 2026



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA PILI – TAREHE 01 APRILI, 2026

I. DUA:

**II. KIAPO CHA UAMINIFU NA AHADI YA UZALENDO
KWA WABUNGE:**

1. Mhe. Fatma Ramadhan Mohamed
2. Mhe. Dkt. Lazaro Killian Komba Bunungu
3. Mhe. Mariam Said Khamis
4. Mhe. Said Ali Mbarouk
5. Mhe. Shaame Ali Ali
6. Mhe. Simai Mohammed Said

III. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI MKUU:

Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko huo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA AFYA NA MASUALA YA UKIMWI:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu (Tume ya kudhibiti UKIMWI Tanzania) kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Ajira, Vijana na Mahusiano) kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

IV. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):

1. MHESHIMIWA KANGI ALPHAXARD LUGOLA (MWIBARA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itakamilisha Maboma 49 ya madarasa ya Shule za Msingi na Maboma matatu ya Zahanati za Vijiji vitatu vya Jimbo la Mwibara.

2. MHESHIMIWA NEEMA GERALD MWANDABILA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, upi mpango wa Serikali katika kuhakikisha Hospitali zote za Wilaya, Vituo vya Afya na Zahanati zinakuwa na Uzio.

3. MHESHIMIWA JACQUELINE NGONYANI MSONGOZI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini ujenzi wa Soko la Mfaranyaki katika Manispaa ya Songea utaanza kwa kuwa hali iliyopo ni hatarishi kwa usalama wa watumiaji.

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

4. MHESHIMIWA RASHID ABDALLAH SHANGAZI (MLALO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, lini ahadi ya kuwapatia maeneo wakazi wa Kata za Lukozi, Shume na Manolo kutoka Shamba la miti Shume itatekelezwa.

WIZARA YA KILIMO:

5. MHESHIMIWA ENOCK ZADOCK KOOLA (VUNJO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Serikali itajenga Skimu za Umwagiliaji kwa ajili ya Kilimo cha chakula katika Jimbo la Vunjo.

6. MHESHIMIWA NAPE MOSES NNAUYE (MTAMA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ipo tayari kupitia upya mfumo wa bei kwenye minada ya Korosho kwa kuwa kuna malalamiko ya namna bei zinavyopatikana.

7. MHESHIMIWA ISSA ALLY MCHUNGAHELA (LULINDI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, tangu kurejeshwa kwa *Export Levy* kwenda Bodi ya Korosho ni kiasi gani kimekusanywa hadi sasa na kimetumikaje.

WIZARA YA MAJI:

8. MHESHIMIWA YAGI MAULID KIARATU (SINGIDA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Chuo cha Maji katika Mkoa wa Singida.

9. MHESHIMIWA ANNE KILANGO MALECELA (SAME MASHARIKI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kupeleka Mradi wa Maji safi Kata ya Mpinji kwa Vijiji vyote vinne.

WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:

10. MHESHIMIWA ESTHER NICHOLAS MATIKO (TARIME MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Kiwanda cha kimkakati ndani ya Mji wa Tarime.

V. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI MKUU:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

DODOMA
01 APRILI, 2026

BARAKA I. LEONARD
KATIBU WA BUNGE

